

## Maswali

1. Paulo alisema nini yenye ilikuwa ngumu Wayahudi hawakutaka kukubali?
2. Mbona kulikuwa na sanamu nyingi kwa barabara za Athene?
3. Waliandika nini kwa hizo sanamu?
4. Nini iliandikwa juu ya sanamu isiokuwa na jina?
5. Paulo alizungumza na nani kwanza alipofika mjini?
6. Mbona Wayunani walimsikiliza Paulo kwa makini?
7. Paulo alianza mazungumzo kwa Wayunani namna gani?
8. Paulo aliambia watu nini juu ya Mungu?
9. Ni nini hasa chenye Wayunani walikataa kuamini?

## Majibu

1. Eti imani kwa Yesu ilikuwa ya maana kuliko sheria za Mungu kupitia kwa Musa.
2. Kwa sababu Wayunani waliamini kwamba kuna miungu wengi. Waliwawekea wote sanamu.
3. Jina la Mungu.
4. “Kwa mungu asiyejulikana.”
5. Kwa Wayahudi.
6. Kwa sababu walikubali kusikiliza maoni ya watu.
7. Alianza kwa kuwambia ni nani ndiye “Mungu asiyejulikana”.
8. Alisema kuna: a. Mungu mmoja; b. Mungu alifanya kila kitu c. Mungu alikubali mwana wake afe kwa ondoleo la dhambi d. Yesu kufufuka kutoka kwa wafu ni thibitisho kwamba Mungu yu hai: e. Mungu atawaadhibu wowote wasiomuamini
9. Hawakuamini kwamba mtu aliyekufa anaweza kutoka kwa wafu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 48 Paulo ako Athene

## Marejeo

Matendo ya Mitume 17:16-34

## Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba kuna Mungu mmoja tu aliyeumba kila kitu. Kuna wakati Mungu atahukumu ulimwengu akisaidiwa na Yesu.

## Maneno maalum

1. Kuzuia (kupinga) + sumbua + gawanya.
2. Athene + hadithi + miungu wengi + sanamu + haijulikani
3. Mungu mmoja + mwana + okoa
4. Mawazi yote
5. Kilima cha kuharibu + watu wengi + kwisha abudu
6. Fanya kila kitu + mtu alichaguliwa + Yesu
7. Cheka + haja

**48.1** Safari ya Paulo ya pili katika utumwa. Alikutana na Wayahudi huko Filipi na Thesolonike lakini hawakukubaliana naye. Hawakukubali kwamba imani kwa Yesu inashinda sheria za Mungu alizowapea kupitia kwa Musa. Lakini watu wa jiji la Beroya walipenda maneno ya Paulo. Walimsikiliza. Watu wa Filipi na Thesolonike walikuja Beroya kusumbua. Marafiki wa Paulo waligawanyika. Paulo alienda Athene.

**48.2** Paulo aliamua mwenyewe kwenda Athene wakati huo. Warumi walitawala karibu ulimwengu mzima. Athene ilikuwa mji wa Uyunani uliyotawala ulimwengu kabla ya Rumi. Athene ilikuwa bado ni jiji la maana. Watu wa huko waliipenda pamoja na historia ya wazee wao. Waliamini kulikuwa na miungu wengi. Sanamu za hawa miungu yote ilikuwa kwa kila njia. Hizo sanamu ziliwakumbusha miungu ni nini. Kila sanamu ilikuwa na jina la kuonyesha ni mungu wa nini. Watu waliogopa kwamba watasahau Mungu kwa hivyo wakamtengezea sanamu. Walitengeneza sanamu na kuandika jina juu yake, “kwa mungu asiyejulikana”



**48.3** Bila kukawia Paulo alitafuta nafasi ya kuambia watu juu ya Mungu aliyewakweli, aliyetengeneza kila kitu. Alitaka kuambia watu juu ya mwana wa Mungu aliyekufa ili waokolewe kutoka kwa dhambi.

**48.4** Kwanza aliambia Wayahudi kuhusu kufufuka kwa Yesu. Baadaye aliambia watu wote waliomsikiliza. Wayunani walikuwa wazuri kwa kusikiliza. Waliona ni vizuri kusikiliza maoni ya kila mtu. Baadaye wangejadiliana maneno waliyosikia.



**48.5** Baadhi ya watu wa mjini walipenda Paulo azungumzie imani yake hadharani. Walimpeleka pahali paitwapo kilima cha Marsi. Kuharibu kulikuwa na watu wengi wakumsikiliza. Paulo alianza na kuambia kwamba, atazungumzia juu ya Mungu wanaomwabudu.

**48.6** Paulo alisema, “Mna sanamu mjini na maandishi, kwa Mungu asiyejulikana. Ninataka kuambia juu yake.” “Yeye ndiye Mungu aliyetengeneza kila mtu. Sisi ni watoto wake, yeye sio sanamu ni Mungu wa kweli. Hatapenda watu wasimjue milele. Kuna siku inakuja. Kwa siku hii amechagua mtu atakaye adhibu watu wenye hawasikilizi. Ametuonyesha kwa kuleta huyo mtu kutoka kwa wafu.” Kawaida alizungumzia juu ya yesu.

**48.7** Mpaka hapo watu wote walisikiliza wakiwa kimya. Lakini Paulo alipoguzia kwamba mtu kutoka kwa wafu, walicheka na wakakataa kumuamini. Lakini wengine wao walikubali na wakamsikiliza mpaka wenzake walipokuja. Wakasikiliza Paulo akizungumza juu ya Yesu.